**HOTUBA YA MGENI RASMI, MHE. DKT. SALIM AHMED SALIM WAZIRI MKUU MSTAAFU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MJUMBE WA JOPO LA WATU WENYE BUSARA LA BARAZA LA AMANI NA USALAMA LA UOMJA WA AFRIKA PIA MJUMBE WA BARAZA LA USHAURI LA UMOJA WA AFRIKA LA MWAKA WA AMANI NA USALAMA WAKATI WA MAADHIMISHO YA MWAKA WA AMANI NA USALAMA BARANI AFRIKA DAR ES SALAAM, TANZANIA, 21 SEPTEMBA, 2010**

**Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa;**

**Mhe. Said Meck Sadiq, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;**

**Waheshimiwa Viongozi mbali mbali wa dini na serikali;**

**Waheshimiwa Mabalozi na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa;**

**Mabibi na Mabwana,**

Nashukuru kwa fursa hii ya kualikwa kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho haya ya mwaka wa Amani na Usalama barani Afrika. Maadhimisho ambayo yanafanyika katika nchi mbalimbali barani mwetu.

Kwa takriban miongo mitatu hivi sasa Umoja wa Mataifa umekuwa ukiadhimisha siku ya amani duniani. Hii inafuatia Azimio la Baraza Kuu la Umoja huo la mwaka 1981 ambalo liliamuru kuchaguliwa siku maalumu ya kuadhimisha juhudi za upatikanaji wa amani duniani kila mwaka na kuanza kuadhimishwa rasmi mwaka 1982. Afrika kama sehemu ya jamii ya kimataifa imekuwa ikiungana na Umoja wa Mataifa katika kuadhimisha siku hii muhimu.

Amani ni msingi wa maendeleo na hivyo ni muhimu kwa nchi yoyote duniani. Bila amani, nchi haiwezi kufanya shughuli za maendeleo. Hata pale ambapo maendeleo yameshapatikana, huweza kuvurugwa endapo amani itatoweka katika nchi.

Leo tunaadhimisha kilele cha Mwaka wa Amani Barani Afrika. Tunaadhimisha mwaka huu kufuatia maamuzi yaliyotolewa na Wakuu wa Nchi na Serikali za Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika. Tarehe 31 Agosti, 2009, Wakuu wa Nchi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete akiwa mmoja wao, walikutana Tripoli, Libya, kwa Mkutano wao maalum ambao ulijadili agenda moja tu muhimu. Nayo ni kuhusu Migogoro Barani Afrika. Viongozi wetu wakiwa na nia ya kutaka kuona watu wote barani Afrika wakiishi kwa amani na

uslama, ikiwa ni pamoja na vizazi vinavyokuja, walipitisha Azimio la Tripoli lililoazimia kuwa mwaka 2010 uwe Mwaka wa Amani na Usalama Barani Afrika. Kauli mbiu ya mwaka huu wa amani barani Afrika ni "MAKE PEACE HAPPEN" au kwa lugha yetu ya Kiswahili, "Fanya Amani Iwepo". Lengo likiwa ni kuongeza msukumo katika jitihada za kuleta na kudumisha amani.

Hivyo, ili kufanikisha maadhimisho ya mwaka huu wa amani na usalama, Umoja wa Afrika umehimiza Nchi Wanachama wake kuandaa shughuli mbalimbali zenye kutoa ujumbe wa Amani. Aidha, AU iliamua kuwa maadhimisho ya Mwaka wa Amani na Usalama Barani Afrika yafikie kilele leo, tarehe 21 Septemba, siku ambayo huadhimishwa na Umoja wa Mataifa (UN) kama siku ya Amani Duniani.

Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwashirikisha wadau mbali mbali ili kufanikisha lengo la amani katika bara la Afrika, Umoja wa Afrika umeunda baraza la ushauri wa masuala ya amani ambalo linajumuisha watu mbalimbali wakiwemo wanasiasa na wanadiplomasia ambao wana uwezo na uzoefu mkubwa wa masuala ya amani na usalama barani Afrika. Jukumu la baraza hili ni kutoa ushauri wa pamoja katika juhudi zinazoendelea kusuluhisha migogoro mbali mbali inayoendelea na pia kuepusha migogoro mingine. Pia imechagua mabalozi wa Amani ambao wanatokana miongoni mwa Waafrika Maarufu wakiwemo wanamuziki, wanamichezo na wasanii kama vile Oliver Mtukudzi, Angelique Kidjo, Salif Keita, Abdi Pele, Michael Essen, Manu Dibango na wengineo.

Katika kuadhimisha siku hii ya leo, Umoja wa Afrika umeazimia kufanikisha shughuli mbalimbali ambazo zinalenga kujenga msingi imara wa kufanikisha nia hii ya dhati ya kuondokana na tatizo la ukosekanaji wa Amani na Usalama barani Afrika. Miongoni mwa shuguli hizo ni pamoja na;

1. Leo iwe ni siku ya kusimamishwa kwa mapigano katika maeneo yote ya vita na machafuko barani Afrika. Ni wazi kama itawezekana kusimamisha mapigano kwa siku moja basi pia tutaweza kujenga utamaduni na uwezo wa kumaliza mapigano kwa pamoja.
2. Usambazaji wa misaada, vifaa na utoaji huduma za kibinadamu katika jamii zilizomo katika maeneo ya machafuko na pia katika maeneo mengine ambayo watu wake wanahitaji misaada hiyo
3. Kukaa kimya kwa dakika moja kwa ajili ya upatikanaji wa amani katika pande zote barani Afrika mnamo saa saba mchana za hapa Tanzania.

4. Kushirikisha majeshi na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika Afrika katika utoaji wa huduma za maendeleo na misaada ya kijamii kama vile usafi wa mazingira, ukarabati wa miundo mbinu, ukarabati wa shule na zahanati, misaada kwa wazee na yatima na kadhalika.
5. Kufanikisha somo la "hakikisha amani inapatikana" katika shule zote katika siku ya leo ama siku nyingine za mbele kama itakavyoamuliwa.

Hivyo, leo ni siku muhimu na ya kihistoria katika bara letu la Afrika. Ni siku ambayo, kwa mara ya kwanza, bara lote la Afrika litakuwa na dakika moja ya amani. Ni kwa sababu hiyo, nchi yetu, Tanzania, ikiwa mojawapo ya Nchi Wanachama wa AU na nchi yenye amani, leo hii inaungana na nchi nyingine Wanachama wa AU katika kuadhimisha siku hii.

Maadhimisho haya ya siku ya leo, yanatukumbusha wote kuwa bado amani haijatengamaa vya kutosha katika bara letu la Afrika. Na amani inayotakiwa, si amani ya siku moja tu bali ni amani endelevu au amani ya kudumu. Hivyo, usuluhishi wa migogoro unabaki kuwa ni changamoto kubwa inayolikabili barani letu.

Tunatambua na kutoa pongezi kwa Mhe. Rais Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Wakuu wengine wa Nchi na Serikali wa Afrika kwa juhudi kubwa ambayo wamekuwa wakifanya katika kutafuta suluhu ya migogoro barani Afrika, kwa njia ya amani. Umoja wetu, AU, ambao tangu uzinduliwe mwaka 2002 na Baraza lake la Amani na Usalama (PSC) kuzinduliwa mwaka 2004, nao umefanya juhudi kubwa kutafuta suluhu ya migogoro mbalimbali ya Afrika. Bila kusahau jumuiya ya kimataifa, ambayo nayo imekuwa ikiliunga mkono bara la Afrika katika juhudi zake za kutafuta suluhu ya migogoro. Lakini pamoja na juhudi zote hizo, migogoro imeendelea katika baadhi ya nchi zetu za Afrika na kusababisha maafa makubwa.

Kwa nchi ambazo miaka ya hivi karibuni zimejitahidi kupiga hatua za maendeleo na zinaendelea kufanya jitihada kuhakikisha kuwa zinapiga hatua kubwa zaidi ya maendeleo kwa faida ya wananchi wote, jitihada hizo pia, kwa baadhi ya nchi, zimeathiriwa na migogoro.

Matokeo ya migogoro hiyo, ni mamilioni ya waafrika wasio na hatia kupoteza maisha yao na mamilioni zaidi kujeruhiwa. Pia mamilioni ya watu hususan wanawake na watoto, kupata shida kubwa na baadhi ya watu kukimbia nchi zao na kukimbilia nchi za jirani katika kujaribu kuokoa maisha yao na hivyo kujikuta wakiishi maisha ya dhiki nje ya mipaka ya nchi yao wakiwa wakimbizi. Mwaka 2009, Afrika ilikuwa na

wakimbizi milioni 3, ambayo ni asilimia 20 ya wakimbizi wapatao milioni 10.5 duniani. Aidha, Afrika inakisiwa kuwa ina watu milioni kumi na moja na laki sita ambao wamelazimika kuhama makazi yao kwa ajili ya vita. Kwa maana nyingine kuwa aina ya "wakimbizi" ndani ya nchi zao.

Migogoro pia inasababisha uharibifu au hasara siyo kwa mali binafsi tu bali pia mali za umma. Mali binafsi ambazo watu wanazipata baada ya kufanya kazi kwa bidii na mara nyingine kwa muda mrefu zinaharibiwa wakati wa mapigano au kuachwa wakati watu wanapolazimika kukimbia makazi yao ili kuokoa maisha yao. Vivyo hivyo, mali za umma k.m. miundombinu, ambayo serikali hujitahidi kuijenga kwa fedha nyingi au hata kwa mikopo kutoka nje, nayo pia huharibiwa wakati wa mapigano.

Vile vile migogoro huwa kikwazo kikubwa kwa shughuli za maendeleo siyo tu kwa watu binafsi bali pia kwa Taifa. Fedha ambazo zingeweza kuelekezwa kwenye huduma muhimu ya jamii kama afya, elimu, maji, n.k. fedha hizo huelekezwa katika ununuzi wa silaha. Hivyo, kusababisha nchi za Afrika kutokuwa na maendeleo. Hasara ya kiuchumi inakadiriwa kuwa wastani wa Dola Bilioni kumi na nane kwa kila mwaka sababu ya migogoro.

Hali hii ya migogoro katika bara letu, imelifanya bara la Afrika kujulikana kama bara la mapigano, jambo ambalo ni dhahiri linasikitisha. Hivyo, hatuna budi kuondokana na hali hiyo ya migogoro na kuwa bara huru lisilo na migogoro.

Ni kweli kuwa katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na mabadiliko ya kutia moyo. Kutokana na juhudi zilizofanyika, Afrika imefanikiwa kupunguza idadi ya migogoro kuliko ilivyokuwa katika miaka ya 1990, wakati ambapo nchi nyingi zilikuwa na migogoro. Nchi kama Liberia; Sierra Leone; Msumbiji; Angola; Rwanda; Burundi; Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Comoro; nazo zimeendelea kuimarisha amani. Hali hii inatupa faraja. Hata hivyo, bado tuna migogoro kama vile ya Somalia na Darfur, huko Sudan.

Mgogoro wa Somalia, ni mgogoro wa muda mrefu sasa. Mgogoro huu ni changamoto kubwa kwa bara letu na kwa jamii ya kimataifa kwa jumla na hivyo unahitaji kuangaliwa kwa umakini zaidi. Hali ya usalama nchini Somalia ambayo kwa takribani miaka ishirini sasa imekuwa katika mazingira ya kusikitisha na kusononesha, ambapo kwa ujumla usalama wa mwananchi wa nchi hiyo umo katika hali ya hatihati. Miongoni mwa matatizo makubwa ya Somalia ni pamoja njama zinazofanywa na kikundi cha Al Shabaab za kuisambaratisha serikali ya mpito ya nchi

hiyo, mauaji ya kutisha na mateso ya kila aina ambayo – yote hayo yamekuwa ni kama jambo la kawaida. Pia limezuka kwa nguvu tatizo la uharamia. Afrika haina budi kuendelea kufanya juhudi kwa kushirikiana na jumuiya ya kimataifa kupata ufumbuzi wa haraka.

Mgogoro wa Sudan ni changamoto nyingine kwa Afrika. Kwanza kuna tatizo la Darfur ambapo wakaazi wa eneo hilo la Sudan wamekabiliwa na machafuko na maafa. Pamoja na juhudi kubwa zilizofanyika na Umoja wa Afrika kushirikiana na Umoja wa Mataifa na jamii ya kimataifa kwa ujumla, za kuleta masikilizano baina ya serikali na vikundi mbalambali vilivyochukua silaha kupambana na serikali bado mgogoro umeendelea. Mazungumzo ya amani yanayofanyika huko Doha, Qatar bado hayajaweza kupata ufumbuzi wa kudumu ingawa inaridhisha kuwa juhudi zinaendelea.

Pili katika miezi michache ijayo kwa mujibu wa makubaliano baina ya serikali ya Sudan inayoongozwa na chama cha National Congress Party na Chama cha SPLM ya mwaka 2005, kura ya maoni inategemewa kupigwa mwezi Januari 2011 huko kusini mwa Sudan ili kuamua nini wananchi wa kusini mwa Sudan wanataka – yaani kama wanataka kubaki kama sehemu ya Sudan au kujitenga. Lililo muhimu kabisa ni kwamba kura hiyo ya maoni ifanyike katika mazingira ya amani na mazingira ya kuelewana baina ya pande zote mbili kuhusu mustakabali wa Sudan.

Kama uamuzi wa wananchi wa Kusini mwa Sudani utakuwa ni wa kujitenga, maelewano haya yajumuishe utatuzi wa matatizo mbali mbali kama vile suala la mipaka, rasilimali pamoja na mafuta. Mustakabali wa Raia waliopo katika sehemu hizo mbili za nchi hiyo ambayo mpaka hivi sasa ni nchi kubwa kuliko yeyote katika bara la Afrika na pia kuandaa namna ya kushirikiana siku za mbele.

Ningependa pia kusisitiza umuhimu wa kuhakikisha juhudi za ziada zinafanyika ili vyanzo au sababu za migogoro sio tu zinajulikana lakini zinapatiwa ufumbuzi na hivyo kuzuia migogoro mipya kuzuka.

Miongoni mwa vyanzo hivyo ni umasikini uliokithiri, ukiukwaji wa haki za binadamu, ukosefu wa utawala bora, usambaratishaji wa demokrasia, utumiaji wa siasa za ukabila na udini kwa maslahi ya muda mfupi ya wanasiasa, kutoheshimu matakwa ya watu katika uchaguzi na pamoja na uchu wa madaraka usio na kifani.

Ndugu wananchi,

Kwa upande wa nchi yetu, tuna fahari kubwa ya kuwa mstari wa mbele katika kujenga mazingira yetu wenyewe ya kuwa na amani, utulivu na mshikamano na pia katika kusaidia ndugu na majirani zetu na sehemu nyingine za Afrika katika kufanikisha lengo la kuleta amani popote pale inapokosekana.

Katika upeo huo, sote tunajua fika kwamba tumetoa mchango huu kwa hali na mali. Kwa mfano, vijana wetu wa jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika miaka ya nyuma walikwenda Liberia kwa lengo hilo. Na hivi karibuni wanajeshi wetu wamekwenda huko Darfur wakiungana na wanajeshi wengine wa kiafrika na nchi nyingine, chini ya uongozi wa Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa.

Vilevile, viongozi wetu wa kitaifa wameshiriki kutoa michango yao muhimu katika juhudi za kuleta amani. Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ametoa mchango muhimu katika kumaliza mgogoro wa ndugu zetu wa Kenya uliotokana na uchaguzi uliofanyika nchini humo mwaka 2007. Pia Rais mstaafu wa awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ametoa na anaendelea kutoa mchango wake katika juhudi za kurudisha amani na utulivu huko katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na hasa mgogoro wa mashariki ya Kongo.

Viongozi wengine wa ngazi mbalimbali wakiwemo mawaziri na mabalozi wamekuwa wakijishughulisha kwa namna moja ama nyingine katika juhudi kama hizo. Mimi mwenyewe binafsi nimekuwa katika harakati hizo tokea nikiwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika kwa muda wa miaka kumi na mbili na nimeendelea na juhudi hizo baada ya kuacha nafasi hiyo mpaka sasa nikiwa katika nyadhifa mbalimbali.

Sote tumeweza kufanya hivyo kwa kujivunia amani, utulivu na mshikamano wa wananchi wetu. Napenda kusisitiza kuwa ni jukumu la kila mtanzania, vijana kwa wazee, mabibi kwa mabwana, viongozi na wananchi, kuhakikisha kuwa amani yetu inaendelea kudumu. Ni wajibu wetu sote kuhakikisha kuwa amani yetu inaendelea kulindwa na pia amani inapatikana katika maeneo mengine barani Afrika. Ni wajibu wa kizazi chetu kuhakikisha kuwa kamwe haturithishi hali ya kukosekana kwa amani na usalama kwa kizazi kijacho.

Kwa kuhitimisha, naomba kusisitiza kuwa amani ni muhimu sana kwa nchi yoyote. Na kila mmoja barani Afrika, ikiwa ni pamoja na sisi sote tuliopo hapa, tuna wajibu wa kuwezesha amani kuwepo katika bara letu. Hivyo, sote tunapaswa kuithamini siku hii ya leo. Ni matumaini yangu kuwa vikundi na vikosi vilivyo katika maeneo ya mapigano barani Afrika

navyo pia vitaheshimu siku hii na kuitafsiri kwa vitendo kwa kumaliza migogoro hiyo kwa njia ya amani. Inasikitisha bara letu kutangazwatangazwa kama ni bara la mapigano. Hivyo katika muda mchache ujao, kwa mara ya kwanza, tunategemea kuwa na mwito wa amani katika bara zima la Afrika angalau kwa dakika moja. Hii haina maana kuwa leo ndiyo mwisho wa Mwaka wa Amani na Usalama bali hii iwe ni ishara yenye kutia matumaini kuwa bara la Afrika lililo huru bila mapigano hatimaye linawezekana.

**Asanteni kwa kunisikiliza**